

# TAARIFA KWA UMMA

## MRADI PENDEKEZWA WA BOMBA LA KUSAFIRISHA MAFUTA GHAFI AFRIKA MASHARIKI(EACOP)

### (Tathmini ya Athariza kwa Mazingira na Jamii)

Serikali ya Tanzania kupitia Wizara ya Nishati na Madini pamoja na Serikali ya Uganda kupitia Wizara ya Nishati na Maendeleo ya Madini kwa kushirikiana na makampuni ya mafuta ya kimataifa zinakusudia kuanzisha mradi wa uendelezaji, ujenzi, uendeshaji na matengenezo endelevu ya bomba la kusafirisha mafuta ghafi ya petrol yanayo zarishwa kutoka eneo la uvumbuzi wa mafuta la Albertine nchini Uganda, hadi rasi ya Chongoleani iliyopo Kaskazini mwa Bandari ya Tanga Tanzania kwaajili ya kusafirishwa nje kwenye soko la kimataifa.

Bomba litatokea Kaabale nchini Uganda nakupita kilomita 1445 za maeneo yenye mandhari tofauti ambapo kilomita 1149 zitakuwa nchini Tanzania nakuishia kwenye kituo cha kuhifadhi mafuta kitakachowekwa rasi ya Chongoleani; na baada ya hapo mafuta yatapakiwa kwenye vyombo vya kusafirishia kupitia gati na kituo cha kupakia mafuta kisha kusafirishwa kwenye soko la kimataifa.

Kutoka upande wa kusini mwa Ziwa Albert nchini Uganda, bomba litaelekea kusini na kupita sambamba na magharibi mwa Ziwa Victoria, litavuka mpaka na kuingia mkoani Kagera na kuendelea likipita mwisho wa kusini ya Ziwa Victoria katika sehemu za mikoa ya Geita na Shinyanga; baada ya hapo litaelekea mashariki kupita mikoa ya Tabora, Singida, Dodoma, Manyara na kuishia pwani ya mkoa wa Tanga.

Mradi wa EACOP pia utahusisha ufungaji / usimikwaji wa vituo juu ya ardhi ili kuwezesha mtiririko mzuri wa mafuta ghafi ikiwani pamoja na vituo vya kusukuma mafuta kutoa joto na vituo vya kupunguza msukumo. Vituo kadhaa vya muda mfupi vya kusaidia ujenzi wa bomba ni pamoja na kambi za ujenzi na maeneo ya kuhifadhi mabomba, kituo cha kufunika mabomba na barabara.

Kampuni ya wataalamu waelekezi ya RSK Group Ltd ya Uingereza kwa kushirikiana na kampuni za JSB Envi-Dep Ltd na COWI Tanzania Ltd za Dar es Salaam Tanzania, zinafanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii (TAM) zinazoweza kutokana na mradi pendekezwa kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura ya 191 ya mwaka 2004.

Hivyo basi Wizara ya Nishati na Madini inatoa taarifa kwa wadau wote kutoa maoni, dukuduku mapendekezo na masuala yoyote yanayohusiana na mradi huu ili yaweze kuzingatiwa kwenye mchakato wa TAM na kubainisha njia za kupunguza athari ili kuhakikisha mradi unaendelezwa bila kusababisha athari kwa mazingira na jamii. Masuala yote yawasilishwe kwa hawa wafuatao hapo chini:

- Katibu Mkuu, Wizara ya Nishatini Madini,  
Barabara ya Kikuyu; S.L.P.422, 40474 Dodoma, Tanzania  
Simu:+255 26 2322017; Fax:+255 26 2320148; Barua pepe: ps@mem.go.tz  
Mhusika: Mratibu wa Mradi: Bwn.Salum Mnuna; Simu: +255 767 457817  
Barua pepe:salum.mnuna@mem.go.tz
- Mkurugenzi Mkuu, Baraza la Taifiti la Usimamizi wa Mazingira (NEMC),  
Mtaa wa 35 Regent; S.L.P. 63154, 11404 Dar es Salaam, Tanzania  
Simu: 022 2774889; +255 713 608930; Fax: 022 2774901,  
Barua pepe: nemc@nemctz.org
- Mradi wa EACOP,  
Total East Africa Midstream BV,  
Kwaja: 369, Kilwa House, Gruf chini, Barabara ya Toure Oysterbay, Dar es Salaam, Tanzania.  
Mhusika: Bwn. Patrick Eyraud,  
Simu: +255 699 832 200,  
Barua pepe:patrick.eyraud@total.com
- Washauri elekezi wa TAM
  - o RSK Group Ltd, Spring Lodge, 172 Chester Road, Helsby UK; WA6 0AR  
Simu: +44 (0)1928726006, Fax: +441928725633; Barua pepe:communications@rsk.co.uk;  
Tovuti:www.rsk.co.uk;  
Mhusika :Bwn. Tim Newton, Simu: +255 744 588 729; Barua pepe:newton@rsk.co.uk
  - o JSB- EnviDep Ltd, Ubungo Plaza Gruf 5, Barabara ya Morogoro; S.L.P. 32312,Dar es Salaam;Simu ya mezani:+255022 2461261; Simu: +255 757 768737; Barua pepe:envidep@gmail.com;info@jsbenvidep.com; Tovuti:www.jsbenvidep.com;  
Mhusika: Bibi. Saada Juma; Simu: +255 754 291997; Barua pepe: skatangi@hotmail.com
  - o COWI Tanzania Ltd, Jangid Plaza Gruf 2, Chumba na 201, Kwaja G6, Barabara ya Chaburuma, S.L.P. 1007, Dar es Salaam; Simu: +255 222666161; Barua pepe:cowi@cowi.com; Tovuti:www.Cowi.com; Mhusika: Dkt. Mathew Richmond; Simu: +255 754 222410; Barua pepe:matt@cowi.com